# MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA, 2020)



**Dondoo muhimu za msimu wa mvua za Vuli kipindi cha Oktoba – Disemba, 2020**

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mwelekeo wa msimu wa mvua za vuli kipindi cha Oktoba - Disemba 2020, ushauri na tahadhari kwa wadau wa sekta mbalimbali kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na uvuvi, maliasili, wanyamapori na utalii, nishati na maji, usafirishaji (nchi kavu, kwenye maji na angani), mamlaka za miji, afya pamoja na menejimenti za maafa. Utabiri huu ni mahsusi kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Nyanda za juu kaskazini mashariki, Pwani ya kaskazini, Ukanda wa Ziwa Viktoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma). Kwa muhtasari, mwelekeo huo na athari zake unaonesha kuwa:

**a) Mvua za Vuli, 2020**

i. Mvua za Vuli zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani na zitakazoambatana na vipindi virefu vya ukavu katika maeneo mengi ya nchi.

ii. Mvua za Vuli zinatarajiwa kuanza kwa kuchelewa kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2020 katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki, na ukanda wa pwani ya Kaskazini pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Morogoro.

**b) Athari zinazotarajiwa**

i. Upungufu wa unyevunyevu katika udongo unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi.

ii. Kujitokeza kwa magonjwa ya mlipuko, kutokana na upungufu wa maji safi na salama.

iii. Upungufu wa malisho na maji unaweza kujitokeza hivyo kusababisha kujitokeza kwa migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

iv. Uwezekano wa kutokea matukio ya moto katika mapori na misitu, hivyo mamlaka husika zinashauriwa kupanga mikakati mahsusi ya kukabiliana na hali hiyo.

**(I) MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA KIPINDI CHA OKTOBA – DISEMBA, 2020**

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa ilivyo kwa sasa na inavyotarajiwa kuwa kwa kipindi cha Oktoba – Disemba, 2020 (*kipengele II cha taarifa hii*), mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya ukanda wa Ziwa Viktoria, nyanda za juu kaskazini mashariki, pwani ya Kaskazini pamoja na maeneo ya Kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya ya Kibondo, Kakonko na Kasulu).

1. ***Mvua za Vuli***

Msimu wa mvua za Oktoba – Disemba (Vuli) ni mahsusi katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka ambayo ni nyanda za juu kaskazini-mashariki, pwani ya Kaskazini pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba, ukanda wa Ziwa Viktoria pamoja na Kaskazini mwa mikoa ya Kigoma na Morogoro. Katika msimu wa Vuli, 2020 mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka.

***1.1 Kanda ya Ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Shinyanga) pamoja na Kaskazini mwa mkoa wa Kigoma:***

Mvua zinatarajiwa kunyesha kwa kiwango cha chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi na zinatarajiwa kuambatana na vipindi virefu vya ukavu. Mvua hizi zinatarajiwa kuanza wiki ya pili ya mwezi Septemba, 2020 katika mkoa wa Kagera na kutawanyika katika mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Simiyu, Shinyanga na Kaskazini mwa mkoa wa Kigoma katika wiki ya tatu ya mwezi Septemba, 2020 na zinatarajiwa kuisha mwezi Januari, 2021.

***1.2 Ukanda wa Pwani ya Kaskazini: (Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na Kaskazini mwa mkoa wa Morogoro):***

Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kunyesha kwa kiwango cha chini ya wastani hadi wastani na zinatarajiwa kuanza kwa kuchelewa katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2020 na kuisha katika wiki ya nne ya mwezi Disemba. Aidha, mvua za Vuli zinatarajiwa kuambatana na vipindi virefu vya ukavu katika maeneo mengi.

*1.3 Nyanda za juu Kaskazini Mashariki: (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):*
Mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi. Mvua hizi zinatarajiwa kuanza kwa kuchelewa katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2020 na zinatarajiwa kuisha mwezi Januari, 2021. Aidha, vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa katika maeneo mengi.







| | |
|---|---|
| *Mwelekeo wa mvua katika msimu wa Oktoba hadi Disemba 2020.* | *Wastani wa muda mrefu wa mvua za mwezi Oktoba hadi Disemba* |

***Angalizo:***
*Ingawa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo machache.*

## (II) MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki liko chini ya wastani na inatarajiwa kuendelea kuwa hivyo katika kipindi chote cha msimu wa Oktoba – Disemba 2020. Hali hii inatarajiwa kupunguza nguvu ya mifumo inayosababisha mvua katika maeneo mengi yapatayo misimu miwili ya mvua kwa mwaka hapa nchini. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika maeneo ya upande wa magharibi mwa Bahari ya Hindi wakati upande wa mashariki mwa Bahari ya Hindi unatarajiwa kuwa na joto la bahari la juu ya wastani. Hali hii

inatarajiwa kupunguza msukumo wa upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki mwa nchi. Aidha, joto la wastani hadi juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika maeneo ya kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kuendelea katika kipindi chote cha msimu wa Oktoba – Disemba 2020 na hivyo kupunguza msukumo wa upepo wenye unyevunyevu kutoka katika misitu ya Kongo kuelekea katika maeneo mengi nchini.

## (III) ATHARI NA USHAURI

Taarifa ya athari na ushauri imeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika tarehe 3 Septemba, 2020.

### a) Kilimo na Usalama wa Chakula

Upungufu wa unyevunyevu katika udongo unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi. Aidha, visumbufu vya mazao na magonjwa vinatarajiwa kuongezeka. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukuaji hafifu wa mazao na uzalishaji kupungua. Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu na mazao yanayoweza kukomaa ndani ya muda mfupi. Mbinu na teknolojia za kilimo himilivu za kuhifadhi unyevunyevu na maji zinashauriwa kutumika. Wakulima wanashauriwa kupata ushauri kutoka kwa maafisa ugani juu ya namna bora ya kuendesha kilimo kwa usalama wa chakula na lishe. Mamlaka husika zinashauriwa kuweka mipango tahadhari na kutoa elimu na ushauri kwa wakulima juu ya njia bora na namna ya kutumia kiwango kidogo cha mvua kinachotarajiwa pamoja na matumizi mazuri ya chakula kilichopo.

### b) Mifugo na Uvuvi

Hali ya kupungua kwa magonjwa ya mifugo na mazao ya uvuvi kama samaki na mwani inatarajiwa. Mtiririko hafifu wa maji unatarajiwa kusababisha uzalishaji mdogo wa mazao ya samaki na mifugo. Aidha, kutokana na upungufu wa malisho na maji kuna uwezekano wa migogoro baina ya wakulima na wafugaji kujitokeza. Wafugaji na wavuvi wanashauriwa watumie utabiri wa hali ya hewa na kufuata ushauri wa maafisa ugani.

### c) Utalii na Wanyamapori

Upungufu mkubwa wa malisho na maji kwa wanyamapori katika mbuga unaweza kusababisha migogoro kati ya sekta husika na jamii wakati wanyamapori wanapotafuta malisho na maji. Aidha, kuna uwezekano wa kutokea kwa magonjwa ya mlipuko kwa wanyamapori kutokana na ukosefu wa malisho na maji. Hali ya hewa inayotarajiwa, inaweza kupelekea magonjwa ya wanyamapori kusambaa kwa wanyama wanaofugwa kutokana na wanyamapori kuingia katika makazi ya jamii zinazozunguka hifadhi na mbuga. Mamlaka husika zinashauriwa ziendelee kutoa elimu kwa jamii husika. Aidha, jamii inayozunguka mbuga itoe taarifa mapema kwa sekta ya wanyamapori pindi wanyama wanapokuwa wameingia katika maeneo yao.

### d) Usafirishaji

Kutokana na utabiri huu sekta ya usafirishaji inatarajiwa kunufaika hususan katika usafiri wa anga na nchi kavu. Sekta husika wanashauriwa kutumia muda huu kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji hasa kwa ujenzi unaohusisha maeneo yanayoathiriwa na mafuriko. Aidha, watumiaji wa bahari wanashauriwa kufuatilia na kutumia taarifa za utabiri wa matukio ya vimbunga pindi utakapotolewa.

### e) Nishati, Maji na Madini

Kutokana na utabiri huu upungufu kidogo wa kina cha maji kwenye mabwawa unatarajiwa, hali hiyo itapunguza changamoto ya mabwawa kujaa maji kupita kiasi. Hata hivyo maandalizi ya nishati mbadala za umeme yanashauriwa ili kukabiliana na upungufu endapo utajitokeza.

Upungufu wa maji kwa matumizi ya nyumbani unaweza kujitokeza kutokana na mvua chache na za muda mfupi zinazotarajiwa. Hivyo, matumizi sahihi ya maji kwa ajili ya uchakataji wa madini, umwagiliaji, matumizi ya majumbani pamoja na kuendesha mitambo ya umeme yazingatiwe.

**f) Mamlaka za Miji**

Kutokana na matarajio ya upungufu wa mvua, mamlaka za miji zinashauriwa kutumia fursa hiyo kuboresha mifumo ya usambazaji wa maji safi na taka pamoja na kuhakikisha kuwa mifumo na njia za kupitisha maji zinafanya kazi katika kiwango kinachostahili.

**g) Sekta ya Afya**

Magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza, kutokana na upungufu wa maji safi na salama. Hivyo, ushauri unatolewa kwa mamlaka husika na jamii kwa ujumla kuchukua hatua stahiki kupunguza athari za kiafya zinazoweza kujitokeza. Aidha, jamii inaaswa kuhakikisha hakuna mazalia ya wadudu wanaosababisha magonjwa kwa kuyaharibu na kuimarisha usafi wa mazingira. Pia jamii inashauriwa kupata elimu ya afya kwa ujumla ili kujikinga na magonjwa mbalimbali.

**h) Menejimenti za Maafa**

Kuna uwezekano wa kutokea matukio ya moto katika mapori na misitu, hivyo mamlaka husika zinashauriwa kupanga mikakati mahsusi ya kukabiliana na hali hiyo. Aidha, hatua stahiki za maandalizi na mbinu za kukabiliana na upungufu wa mvua ziendelee kuchukuliwa.

**i) Vyombo vya habari**

Ushauri unatolewa kwa vyombo vya habari kufuatilia mara kwa mara na kusambaza taarifa sahihi za mwenendo wa hali ya hewa na mirejeo inayotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA). Wanahabari wanashauriwa kutafuta na kutumia maelezo ya wataalam wa sekta husika katika kuandaa na kufikisha taarifa za masuala mtambuka ya hali ya hewa kwa jamii.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

*Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo vitazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania.*

**Mamlaka ya hali ya hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua nchini kadri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahsusi za utabiri wa msimu ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.**

Imetolewa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania:

Tarehe 08 Septemba, 2020